And also, special schools to be established in every district because right now we have some districts with those schools and here in Nandi for example, we have got only one special school, that is Kapsabet school for the deaf. We should also have a school for the blind, a special school also for the mentally handicapped or those who are mentally retarded. And then also, job opportunities. You find that there is a lot discrimination when it comes to giving job opportunities, jobs to those who are disabled. Because we have those who are educated they have gone upto university level, but they are not considered. And then also, another point is on political arena. When I go to political arena now for those people, in the civic elections, the disabled persons should be given 10% we presentation to start with.

And then for parliamentarians they should be given about 10% of the seats should be reserved for those people. Because they are what I can say endangered species. And.....(Inaudible).

Com. Ayonga: Mwisho?

Mr. Ashon Kosgey: I also would like to say that if that is not going to be done, I think you are going to implement on that because we have suffered for a long time we the disabled persons,

Com Asiyu: Faith, have faith.

Mr. Ashon Kosgey: yes, we have faith; we cannot be beggars for along time.

Com. Ayonga: Okay,

Mr. Ashon Kosgey: We are now reaching a state whereby we are saying enough is enough.

Com. Ayonga: Okay

Mr. Ashon Kosgey: So, thank you Mr. Commissioner,

Com. Ayonga: Thank you sana, habu kuja hapa ujiandikishe Joshua Ruto yuko?

Com. Asiyo: Mary Kojo.

Com. Ayonga: Kuna mama anaitwa Mary Kojo? Kuna mama anaitwa jina hilo? Je, kuna mama yeyote. Hapa sasa nitatumia uwezo wangu wa kiti. Kuna mama yeyote hapa aliye na jambo linamchoma roho yake? Kuja hapa mbele tukupe nafasi uende kutafuta mboga.

Speaker: Tuko wawili.

Com. Ayonga: Kama mko wawili kuja mwingine asimame hapa mwingine akigonjea. Tena kuna mama mwingine. Nataka kufukuza wa mama waende nyumbani. Kuwafukuza, mkipenda kukaa sawa lakini mapigo ni yako jioni.

Com. Asiyo: Okay, you can take the mic.

Ms. Marion Cherop Mustafa: Asante sana kwa nafasi hii.

Com. Ayonga: Sema majina,

Ms. Marion Cherop Mustafa: Mimi ni Marion Cherop Mustafa.

Com. Ayonga: Okay, endelea.

Ms. Marion Cherop Mustafa: Ningependa kusema ya kwamba, kuna mambo mengine kama rape cases. Hatupaswi sisi wanawake, rape cases, mwanaume aende achukuwe au a-handle hiyo kesi. Tunataka mwanamke kama sisi achukue hiyo kesi juu anasikia huo uchungu. Kwa hivyo andika hiyo Bwana Commissioner.

Okay, na kitu kingine ni kwamba, wache niseme ya kwamba Army wa iliandikwa jana. Wanawake ama wasichana rika langu walikuwa wengi sana lakini inahuzunisha ya sana kuonekana kwamba hii Constitution ambayo tuko nayo hawa balance wasichana kwa wavulana. Wasichana wanachukuliwa kuwa yaani hawana faida kabisa. Na wavulana wanapewa hizo nguvu zote, ati akili yote na kila kitu ni chao. Waliandika wasichana wa-nne na wavulina thelathini. Hebu fanya comparison uangalie kama inaezekana katika Constitution. Hiyo tunataka wangeuze, tafadhali.

Com. Ayonga: Unataka wageuzaje?

Ms. Marion Cherop Mustafa: Wageuze, wafanye kama ni kuandika wasichana kumi, waandike wavulana kumi na wawili.

Com. Ayonga: Na kwa nini wavulana wanakuwa kumi na wawili na wasichana wanakuwa kumi, mbona husema kumi kumi?

Ms. Marion Cherop Mustafa: Kwa sababu kwa sasa, wameandika wavulana ishirini na wangapi? Na wasita na wasichana ni wanne. Kwa hivyo kwa sababu wamejichukulia kuwa zaidi kuliko wasichana, wacha tuwalete karibu karibu, hivi karibu tutakuwa ten ten.

Com. Ayonga: Okay, thank you.

Ms. Marion Cherop Mustafa: Na kitu kingine ni kwamba, inatakikana watu kama mad people, yaani wale ambao wako akili pungwani,

Com. Ayonga: Okay,

Ms. Marion Cherop Mustafa: Wapewe free education, free treatment, yaani kila kitu ikuwe free hata kama wataweza kusoma mpaka university.

Com. Ayonga: Okay,

Ms. Marion Cherop Mustafa: Na Nyayo Tea Zone, kama Nandi Nyayo Tea Zone, ikuje Kapsabet County Council, watoto wetu wasome free, na tupewe medical care free 75% of the money should remain with the county council.

Com. Ayonga: Hebu sema ya mwisho.

Marion Cherop Mustafa: Okay, wacha nimalize,

Com. Ayonga Ya mwisho

Marion Cherop Mustafa: Ya mwisho ama karibu na mwisho?

Com. Ayonga: Aa aa,. Ya mwisho.

Marion Cherop Mustafa: Okay, ningependa kusema ya kwamba, kama retirement ya President, ningependa kusema ya kwamba in our next Constitution, ingepaswa apewe benefits, allowances na good security.

Halafu another thing is freedom of movement. Mambo ya kusema ati haitakikani mtu a a-move usiku wala mchana, tunataka freedom of movement. Na hiyo mimi naweza kuenda mahali popote wakati wowote.

Com. Ayonga: Thank you.

Marion Cherop Mustafa: Nita malizia kusema ya kwamba, no smocking in public, hiyo tumekataa. Thank you.

Com. Ayonga: Asante, hiyo ndiyo point ambayo hakuna mtu alikuwa amesema. Lakini hii kutembea usiku na mchana, tutalala sasa gani na kwenda kazi saa gani?

Mrs. Rodah Serem: Yaah, I have few views about the Constitution,

Com. Ayonga: Tafadhali tumsikie mama, hiyo pia ni moja wapo ya mambo ya Constitution. The freedom ya kuachia mtu aseme apendavyo.

Mrs. Rodah Serem: I want the adaptation of a two party system in our country, where we have only one legal opposition political party. Which is not just doomed to opposition, but has chance to get power and this will enable the existing party in power to be responsible and fulfil the needs of the citizens.

Two, I want the adaptation of a federal system of government.

Three, I want residential system of government again, with the office of the Premier to assist him in his executive powers. And the presidential election should be separated from the general election. That is the separation of elections.

Speaker: Inaudible,

Mrs. Rodah Serem: So, that at one time, the electorate, just look up to one person, that is the President.

Thirdly, I wasn't a specific seats be reserved for interest groups. Like the religious group, the handicapped, the educationists, the trade unionists. Maybe I can say about 4% of the seats in Parliament.

Another one is that I want the duties, the functions and the powers of Members of Parliament be clearly defined by the Constitution. Whereby when we elect a Member of Parliament, we know the powers they have, we know the functions they are supposed to do, so that we can have a ground when can see our MP is not doing work. What work have you assigned him to do? So we want the law, the Constitution to define those responsibilities. Again, we want the office of the Members of Parliament to be in the constituencies so that we don't have to go the MP's house to look for him. We will have to get him in his office.

Again, the Members of Parliament, the money they earn is too much for a part time job. So, Members of Parliament, responsibilities should be full time, because that is too much money when some of us are earning very little money for full time responsibilities.

So, their responsibility should be full time and that will make us get access to him because he will always be in the office when he is not in Parliament.

In customary laws, I want a penalty that is going to get the sorcerers and the witches. You know when the Lancaster House conference was made, the white man and the few Africans who were there overlooked the idea that the Africans have sorcerers. So when we get witchcraft in our community we cannot take him to a law court because there is no law that criminalizes that person. So because we are Africans we know there are witches in our society, we need a penalty that is going to fix this person. I also want the recognition of indigenous land rights because this is an area where we have seen so much violation of the indigenous land rights in our country and.

Com. Pastor Ayonga: Okay, finally.

Speaker: Finally I want compulsory, free primary education.

Finally, women to women marriage to be outlawed.

Com. Pastor Ayonga: Mmesikia vile mama amesema? Ndiyo. Mama sema majina yako.

Jane Sawe: *Kigurenon Jane Sawe*

Translator: Anaitwa Jane Sawe.

Jane Sawe: *Neta*

Translator: La kwanza.

Jane Sawe: *kiabore ane civic education konyolu koribi imandab kwonyik.*

Translator: She says the way she was taught in the civic education was that there are some laws they want to write to safeguard the rights of the women.

Jane Sawe: *Anan ko bik che kere kwonyik che kigitun koma ki .*

Translator: For certain groups of people do not see the married women as anybody.

Jane Sawe: *Ago en katunisiet kokiikogimwachi chechang kou ole bo kechamdoak kotoretige.*

Translator: And during marriage they were promised a lot, that they will be loving each other, they will be assisting each other.

Jane Sawe: *Ago ye kagosirto betusiek kebir kwondo anan okot kicher konda anan ko kit neu non.*

Translator: Then after a short while the woman is beaten and may be even gorge out the eye or chop off the hand or something like that.

Jane Sawe: *Ko nyolu komi ngatutiet neribe kwonyik.*

Translator: So they want some laws which will safeguard and protect the women.

Com. Pastor Ayonga: Mama, we want those laws from you. You tell us exactly what you want.

Jane Sawe: *Amache kesir ngatutiet ne ribe chepyosok asngotebiye lagok kogere mama ago baba nin mamache ale aboi boyot kou yon ibwati bik alage .*

Translator: She is saying she wants the law which will make the husband respect the wife and the wife to respect the husband.

Jane Sawe: *Amun olinyon nandi komawendi boiyot kichen kokwonye .*

Translator: Because traditionally here there is no day when the husband will go to the kitchen to cook when the wife is just sitting.

Jane Sawe: *kimila komami boiyot konyone chiget ak kogugureni tuguk che mi ma.*

Translator: Traditionally, the man is actually somebody who will guard and protect the house when the wife is in the house cooking.

Com. Pastor Ayonga: So you want men to get into the kitchen and start cooking?

Translator: No.

Jane Sawe: *Amache kityok ngotepchei kongen kole achito makonemwan konda ago kinanyoneen konyo abo konyek tuwan.*

Translator: What she wants is the husband to do is to respect the wife.

Speaker: Prevention of domestic violence

Jane Sawe: *Ngolyot age kolole kipcheitoi tuguk kemi ko kora komatagitun cheptanyun ago kiosich werik ak tibik.*

Translator: The next thing is about the property. When they are sharing the property in the house, there are some girls within the family who are not married.

Jane Sawe: *kokmatagitun chepto nyun komamache kigochi tuguk nusu ak werikyu amun kiasiche twan*

Translator: She is saying, if the girl is not married she should get access to equal inheritance like the boy.

Jane Sawe: *Angot ko korenyon ko egarinik tiptem anan ko mut anana k ata kigochin chepto poindit ne ngole kobat komatinye libati ko ngole koyaga tuga komami ole kiyagen.*

Translator: Even when dividing land, it should be divided among all children, the girls and the boys alike.

Com. Pastor Ayonga: Mama umemaliza? Nataka nikuulize kitu kimoja, mama umeongea vizuri toka wakati wa harusi, mimi nimeshafanyia watu wengi harusi na ningali ninafanyi watu harusi na wana-pledge na wanasema watafanya hivi na vile na vile na hiyo itaendelea ikiwa kuna upendo kati ya hawa watu wawili. Sasa jambo hili la domestic violence, hii vita kwa nyumba ambavyo tungalipenda kuona Constitution ambayo inaleta kuheshimiana katika nyumba. Unajua wanaume hawa, mara nyingi tunapongea neno domestic violence, we tend to think it is man against woman.

Translator: *Kole boriet ne imuchi komi ko kobortos boiyotak chepyoset kale mi boisiek che kimuche kebire chepyosog lakini mamwae*

Com. Pastor Ayonga: Lakini experience tells us kwamba hii domestic violence wanaume wengi hapa wako wale ambao wanapigwa na mabibi lakini wanaume hawa hawawezi kusema mbele ya wanaume wenzao kwamba wanapigwa.

Com. Pastor Ayonga (Interjection): Kwa hivyo ulimwengu unazidi kufikiri kwamba wanaume wanapiga wanawake lakini wanaume hawapigwi. Ninajua, hata wewe unajua hivyo, wanawake mnapokuwa katika mabaraza yenu mnasema kale nikikafinya hakatasema. Tungalipenda kuona Constitution ambayo watu wote, equality hii iwe kwamba hakuna mwanaume anayemtendea mwanamke vibaya na mwanamke pia asitende mwanamme vibaya. Kwamba tuwe na amani katika nyumba kuliko kufikiria kwamba domestic violence means a man beating his wife.

Jane Sawe: *au konamege rtet ak teta kigayai ne kikebir noton.*

Translator: Anasema the cow and the goat are not equal.

Com. Pastor Ayonga: Tena angalia kitu umeongeza, umekuja ukafanya mwingine mbuzi mwingine umefanya ng'ombe.

Jane Sawe: Kwa sababu hawa sio sawa kwa nguvu zao.

Com. Pastor Ayonga: Wacha mama mwingine akuulize swali.

Com. Phoebe Asiyu: Ningependa sana utusaidie Mrs Sawe kwaa jambo ambalo umetaja lakini hukutaja mpaka mwisho. Kuna kuwa na wakati msichana na kijana wanaowana halafu wakishakaa kwa muda, mtu anaweza kuleta bibi wa pili. Hii inafanyika hata hapa Nandi si ndiyo? Nataka utusaidie, ningependa utueleze kabisa kama bwana wakati ule anakuo, kama anajua kwa nia yake kwamba wakati mwingine ataweza kuleta bibi mwingine akuambie kwamba ana... tufanye mpango kwa Katiba kwamba kuna potentially polygamous system of marriage at the time of marriage na akueleze kwamba anakuo under this particular system of marriage ili ujue tu ukiolewa kwamba wakati mwingine bibi mwingine anaweza kuja.

Tena tuwe na ile ya wakristo ambao inaonekana wanaambiwa wasioe lakini wanao tu, na bibi wao hawawapeleki kotini. Hata ile ya DC wanafanya namna hiyo, wengine wanao kwa njia ya Kinandi. Hii ndoa ya Kinandi ili mambo yawe sawa, unaona ni vizuri msichana aelezwe akiolewa kwamba, you are being married under a potentially polygamous system of marriage?

Translator: *kegas chon*

Jane Sawe: Hiyo si lazima hata kwa Kinandi si ati ni lazima aoe bibi wa pili.

Com. Phoebe Asiyu: Lakini unajua sisi hapa Kenya tulisema kwamba polygamy iwe abolished na Bunge ilikataa na Tanzania waliandika vile vile tulisema na hakuna polygamy katika Tanzania sasa hapa Kenya unataka namna gani?

Jane Sawe: Hapa Kenya nataka iwe kama ya Kanisa. Kwa sababu kwa bibilia tunapooana, tunasema mpaka wakati wa kifo ndio itetutenganisha.

Com. Phoebe Asiyu: Kwa hivyo tusema hakuna polygamy tena Kenya hii? Tuseme hivo? Hata wezee wamekubali hiyo jambo? Okay, sawa sawa.

Com. Pastor Ayonga: Lakini mama, mbona umeogopa kusema hili neno.

Jane Sawe: Kama?

Com. Pastor Ayonga: Jambo umeulizwa ni kwamba tuseme katika Kenya hakuna polygamy?

Jane Sawe: Ndiyo.

Com. Pastor Ayonga: Mbona husemi hivyo?

Jane Sawe: Hakuna mwanamke wa pili.

Com. Pastor Ayonga: Hakuna mwanamke wa pili.

Jane Sawe: Asiolewe akiolewa shauri yake.

Com. Phoebe Asiyu: Thank you very much.

Jane Sawe: Sikuwa nimeelewa, hakuna haja ya mwanamke wa pili yeye si kifo ya nyumba yetu.

Com. Phoebe Asiyu: Asante sana. Wale wameoa wakae na wao lakini wale hawajaoa wasioe bibi wa pili.

Com. Pastor Ayonga: Kuna mama mwingine?

Speaker: Ndio huyu.

Com. Pastor Ayonga: Yes, but I want to know whether there is another. Ama huyu ndiye wa mwisho? Nataka kuita mama mwingine. Kuna mama mwingine kule kati ya watu? Angalia nimetumia ile lugha mbaya kati ya watu.

Com. Phoebe Asiyu: She is the last one. Endelea mama.

Jane Toroitich: *Abaibai amun kwonyik nguni*

Translator: She is saying she is happy because women now.....(inaudible)

Com. Pastor Ayonga: Majina yake kwanza?

Jane Toroitich: Jane Toroitich.

Translator: Jane Toroitich.

Com. Pastor Ayonga: Endelea mama Jane.

Jane Toroitich: *Konyonireyu si amwa agobo rival KCC.*

Translator: She is saying she has come here, she wanted the revival of the KCC.

Jane Toroitich: *Amun yoton ko olkiginyorunen rabinik.*

Translator: Because that was their way of earning some money.

Com. Phoebe Asiyo: Ingine?

Jane Toroitich: *Amache sokoni ne amuche aaldaen rurutikab imbaret.* (Vernacular)

Translator: She wants a market to sell her produce from the farm like maize.

Jane Toroitich: *Asome kora kisip kotini konyo ireyu.*

Translator: Anaomba tena koti ije karibu hapa.

Jane Toroitich: *kongoi*

Translator: Thank you.

Com. Pastor Ayonga: Asante sana mama, *kongoi kongoi mising, kongoi.* Ujiandikishe mama. Kuna mama yoyote. Nataka akina mama waende nyumbani. Kuna mama yoyote? Sasa ninataka wazee, wazee kabisa. Kama wewe unajijua ni mzee karibu na wale wazee walitajwa waende kulindwa. Mzee unaweza kuingia hapo, chukua moja ya hiyo microphone. Mzee unaweza kuingia hapo, chukua moja ya hiyo microphone.

Speaker: Asante sana mabibi na mabwana kwa kunipa nafasi hii ndogo. (Vernacular)

Com. Pastor Ayonga: Sema majina yako na kama ulianza vizuri na Kiswahili, tena una mfanya nini? Kwa nini wewe unaweza kufanya hivyo? Endelea namna hiyo, ni dakika moja tu.

Speaker: Nimesema asante mabibi na mabwana **Vernacular**

Translator: Anasema he has three points to make.

Speaker: *ne ta*

Translator: First.

Speaker: *konyolu kichuchuch dowery.*

Translator: Anasema the dowry should be reduced.

Speaker: *Yon kamyam chito konyolu koribserkali ak kogochi kerichek chebo buch.*

Translator: He is asking that whenever somebody becomes sick the government should take care of him and give him free treatment.

Speaker: *Yon kimwa agobo maiywek maiywekab chumbek kotindo lesienit ago changaaak local brews komatindo leseaniy.*

Translator: He is saying when you talk of drinks, the European drinks are licenced and they are available but the chang'aa and the local brews are not licenced and they can be arrested at any time.

Speaker: *Amzche kiyam keye changaa ak maiywek ab ka.*

Translator: He wants to be given an okay to drink chang'aa and busaa.

Speaker: **Vernacular.**

Com. Pastor Ayonga: I would like you translator please to say the way he says it not to say he says. Speak as if you were him.

Translator: I am requesting that the fines given when I am arrested after drinking the chang'aa or the busaa should be reduced. The fine should be very low.

Com. Pastor Ayonga: To how much?

(Interjection)

Speaker: By the way, there is something else he has said. He saying he is also being fined for a change he is not aware.

Translator: (Vernacular) that was the first one. The second one he says, I am being fined somewhere before reaching the court.

Com. Pastor Ayonga: That somewhere is what?

Translator: *Ano yoton*

Speaker: *Aarogeni ndamun to konyokobiron kora.*

Translator: I am fearing to say because I might be attacked later on.

Com. Pastor Ayonga: Just a moment, let me assure him. Mzee in this kikao hiki chetu, hakuna mtu atakayekuwa arrested kwa maana amesema his mind. Let me assure you this, if you are arrested today, report it to us. Anybody can report to us for anybody arrested because he or she gave the views, we have that protection.

Speaker: *Bwone polisiek olinyion ak konyogocheng ak kosich maiywek , ago yon kanamin igoini ki kitten.*

Translator: The Police come to our homes and investigate and get the pombe and then when they arrest you, you give them something.

Speaker: *Amache kealda changa en bar ak kee busaa en kaa.*

Translator: I am recommending that the chang'aa should be sold in the bars and the busaa to be drunk at home.

Speaker: *Ane ko a Mwalimu ne kigoretiyaren ago a kenyisiek 76.*

Translator: I am a retired teacher, I am 76 years old.

Speaker: *Abore tos maaonoton amun kimonamankingota Mwalimu.ago kuni korayositu kobwane koamon.*

Translator: I thought they could not be chasing me now because I was not arrested when I was a teacher and now when I am a mzee they come and arrest me when drinking the busaa.

Speaker: *kiawe jela arawek somok ago nguni asomekebagatech.*

Translator: I have been sent to jail earlier on for three months but now I am requesting that we are set free.

Com. Pastor Ayonga: Thank you very much mzee kwa maoni yako.

Speaker: *kongoi.*

Translator: Asante.

Com. Pastor Ayonga: *Kongois, Kongoi mising.* Thank you. Mwalimu sasa weka kidole lakini busaa isije inakusumbua Wacha kunywa hivyo vitu ili Mungu akupe siku nyingi za kuishi.

Paul Chumo: Ningetaka tu kusema machache juu ya yale ambayo yametajwa. Yangu ni kwamba.

Com. Pastor Ayonga: Mzee, umesema majina?

Paul Chumo: Mimi ni Paul Chumo.

Com. Pastor Ayonga: Paul Chumo, okay, endelea.

Paul Chumo: Ningetaka kutaja tu juu ya mawaziri. Kazi ya Mawaziri au Waziri, ateuliwe kulingana na masomo yake kuwa waziri fulani kufuatana na masomo yake. Kama Waziri wa health iwe yeye alikuwa daktari kuliko kuteuliwa kuwa Waziri mtu ambaye alikuwa mtu wa jeshi, ingekuwa bora akiteuliwa mtu ambaye alisomea masomo hayo.

Com. Pastor Ayonga: Hiyo tumesikia, tumepata point.

Paul Chumo: Neno lingine ni ma-Councillors. Councillor ateuliwe mtu ambaye ana miaka arubaine na tano na kuendelea na watu ambao ni wasomi ili kusiwe na mambo ya kuvunjwa kwa ma-Council kila wakati kutokana na elimu ndogo.

Com. Pastor Ayonga: Asante, endelea.

Paul Chumo: Jambo lingine ni kuhusu mambo ya ardhi. Katika Nandi kuna watoto wanaouza mashamba wakipatiwa mashamba na wazazi. Ingekuwa bora au ningeomba uuzaji wa shamba lazima ishuhudiwe na wazazi na watoto.

Com. Pastor Ayonga: Asante sana Paul.

Paul Chumo: Jambo ambalo lina mzozo lifanywe kufuatana na kesi katika division na wale ambao wamechaguliwa kuwa katika panel, panel of elders wachaguliwe watu ambao wana mali ili wasiangukiwe wakati kila na mambo ya *mrungura*. Mnajua maana ya *mrungura* ni nini?

Com. Pastor Ayonga: *Mrungura* ni nini?

Paul Chumo: *Mrungura* ni watu wa kupenda mambo ya chai chai. Wanakamati wa mashamba wale wazee wa panel, wachaguliwe wazee ambao wana maendeleo, wale wazee ambao wana mali yao sio watu ambao wanaweza kuangukia ile

murungura.

Jambo lingine ni kwamba, kamati hiyo panel of elders wachaguliwe akina mama hata na wazee kwa sababu mama hawezi kushika mrungura.

Com. Pastor Ayonga: Asante.

Paul Chumo: Jambo lingine Bwana Commissioner ni kwamba kugawa kwa mashamba, watoto ni sawa sawa. Nilisikia mama akisema watoto ni sawa, kama kuna msichana ambaye amekosa kuolewa lazima apatiwe shamba na wazazi wake na si dhambi kwa baba kumpatia shamba huyu mtoto.

Com. Pastor Ayonga: Hiyo ni kweli tupu.

Paul Chumo: Mambo ya makesi, kuna makesi madogo madogo Bwana Commissioner. Kuna makesi madogo madogo yale ambayo mtu baada ya kupata chakula chake pahali fulani anaenda kwa barabara, pengine anaenda akitota tota namna hii, polisi anasema ingia kwa gari. Mtu anaenda karibu maili sabini, kesho yake hii kesi inahusiana na watu wengi wa kuenda kusikia kesi hiyo au kuenda kule na ni kutoka maili hii. Ingefanyiwa kesi hiyo kwa division.

Com. Pastor Ayonga: Hiyo tumesikia.

Paul Chumo: Jambo lingine tena, hiyo kesi iwe inasaidiwa na wazee wa-chache na akina mama wachache ambao wanahusiana. Ikiwa kuna mama alishikwa, akina mama wataweza kusikiza hiyo kesi.

Com. Pastor Ayonga: Sasa mzee unaweza kutupa hiyo karatasi yako.

Paul Chumo: Kidogo tu. Mambo ya rape, mambo ya raping Bwana Commissioner ingekuwa kama mtu mkubwa amenajisiwa, mwenye kumnajisi apewe miaka ishirini na kama alikuwa mtoto mdogo apewe miaka thelathini na kuchapwa viboko kumi.

Com. Pastor Ayonga: Asante hiyo imetosha. Sasa sikia, mzee jina lako ni nani hapa?

Kiptanui Aramngisire: Kiptanui Aramngisire.

Com. Pastor Ayonga: Ulikuwa umejiandikisha?

Kiptanui Aramngisire: Jina langu liko hapa kwa list.

Com. Pastor Ayonga: Okay, mzee endelea. Tafadhali usichukue muda mrefu.

Kiptanui Aramngisire: Mimi sitachukua muda mrefu.

Com. Pastor Ayonga: Endelea. Sema majina kwanza.

Kiptanui Aramngisire: Nimesema Kiptanui Aramngisire.

Com. Pastor Ayonga: Endelea mzee.

Kiptanui Aramngisire: Vile tulikuja hapa, tulikuja kwa ajili ya Katiba.

Com. Pastor Ayonga: Endelea.

Kiptanui Aramngisire: Mambo ya Katiba nifikiria kama ni kitu cha kupitishwa vile Wanandi wanasema katika hapa Mosop Division.

Neno la pili, kutokea mwaka hamsini na nane mpaka wakati tulinyakuwa uhuru sitini na tatu na wakati tulipata uhuru, tulipata na vyama ngapi? Tulikuwa na vyama viwili au kimoja.

Com. Pastor Ayonga: Wewe ndio unasema.

Kiptanui Arammgisirie: Kwa hivyo ninasema ya kwamba, wakati tulipata uhuru tulikuwa na chama cha KANU na KADU na ninasema mbele yenu, mimi nasema kwa kweli kama mbaya au mzuri. Kitu ambacho kinaleta siasi mingi katika Kenya au Africa ni vyama vingi na dini nyingi. Unasikia mtu anaenda kuhubiri barabarani, ati wewe funga macho halafu mimi nitakuombea halafu upate pesa. Hiyo ni kweli iliundwa hapa Kenya ama iliundwa Nairobi?

Com. Pastor Ayonga: Utuambie unataka aje mzee?

Kiptanui Aramsingirie: Kitu ile mimi nataka Bwana Sambu na nyinyi pamoja.....(Inaudible).

Com. Pastor Ayonga: Hii maneno si ya Bwana Sambu.

Kiptanui Aramsingirie: Sorry.

Com. Pastor Ayonga: Hebu sema umekosea.

Kiptanui Aramsingirie: Nimekosa nisamehe hapo. Mimi nasema Mrs. Asiyo, kitu ile mimi nataka hapa Kenya tulikuwa na dini nne peke yake ambazo tulikuwa tunajua.

Com. Phoebe Asiyo: Ziwe dini nne sasa?

Kiptanui Aramsingirie: Ndiyo, hiyo ni mambo muangalieni, hizo dini nyingi sitaki, ndio inaleta siasa Kenya.

Com. Pastor Ayonga: Na vyama?

Kiptanui Aramsingirie: Vyama tena hiyo ndio inaleta maneno mengine mbaya.

Com. Pastor Ayonga: Unataka ziwe ngapi? Iwe KADU na KADU?

Kiptanui Aramsingirie: KANU yenyewe ndio ilileta uhuru.

Com. Pastor Ayonga: Halafu na KADU tufanyeje.

Kiptanui Aramsingirie: KADU isimame mgongo wake kwa KANU.

Com. Pastor Ayonga: Thank you so much.

Kiptanui Aramsingirie: Siasa mingi ndio imelete taabu nyingi.

Com. Pastor Ayonga: Okay, njoo hapa ujiandikishe.

Com. Pastor Ayonga: Hebu useme majina na uendeleo mzee.

Elija arap Terer: Mimi ni Elijah arap Terer. Yangu ni kuhusu uuzaji wa mashamba. Kumekuwa na mtindo mbaya, mashamba yanauzwa barabarani, yanauzwa hata kwenye pombe na watoto wanauza shamba bila idhini ya baba au jamaa. Na pesa hizi zinapatikana kama mtu ameuza shamba zinapotea kwa pombe. Kwa hivyo ningesema ya kwamba, sheria iandikwe ya kwamba,

kuuza shamba lazima familia wenyewe waka chini wasikizane wauze kwa sababu hii na hii. Sasa kuna uuzaji wa huko na huko na mzee anaweka sahihi, hata nani anaweka sahihi na anapewa pesa kwa kuweka sahihi. Kwa hivyo shamba iuzwe kama familia wamekaa wamesikiza na ipitishwe hata wakija kwa board tena, wote waje na waeleze sababu ya kuuza shamba ni nini. Iliuzwa kwa ajili ya ugonjwa, iliuzwa kwa ajili ya masomo ya kuenda ng'ambo au wapi? Bila sababu hakuna.

Com. Pastor Ayonga: Okay, pointi ingine.

Elijah arap Terer: Haya, jambo lingine, mambo ya mishahara katika Kenya hii, tunasikia hata watu wengine wanapata mishahara sijui milioni ngapi kwa mwezi moja. Nani aliwapatiwa mishahara hiyo? Hata wengine tunasikia hata pengine ni Bunge au County Council wanaketi wana-decide wenyewe mishahara kiasi gani, sisi Councillors tungepata mishahara kiasi gani. Unafikiri wataweka chini? Si wataweka juu hata kama ni Wabunge ndio wanajipitishia mishahara. Lazima kuwe na body katika Kenya ya kupima mishahara ya waalimu ni kiasi fulani, councilors kiasi fulani, wajumbe kiasi fulani, daktari kiasi fulani. Body moja ya Kenya ina-decide salary ya watu wote.

Com. Pastor Ayonga: Ingingine tena mzee.

Elijah arap Terer: Ingingine, kuna magonjwa mabaya mabaya ambayo yanaingia na watu wengi wamekufa kama ugonjwa wa moyo. Unasikia huyu hawezi kutibiwa katika Kenya anataka apandishwe kwa ndege atibiwe South Africa au Ulaya na ni ma-milioni ya pesa. Sasa tutafanya nini? Hata wengine wameweka kwa television, tunataka kiasi fulani, leteni donation. Tunataka cases kama hizo kama magonjwa ya kutibiwa ngambo kama ya moyo na zingine zilipwe na serikali.

Basi jambo lingine, nasisikia mambo ya title deed inaandikwa 99 years, certificate, sijui hata hii yetu ya reserve ni 99 years au ile ya Wazungu peke yake. Kama ilikuwa ya Wazungu hatutaki hizo 99 years hata kama ni a milioni years. Title deed kama imepeanwa, iwe imepeandwa kabisa hakuna la kusema iko na expiry.

Com. Pastor Ayonga: No limit. Okay.

Elijah arap Terer: Basi, mambo ya kuoa, kwa desturi tunakwenda kuomba msichana na jamaa wanakwenda pamoja na yule ambaye anaoa. Sasa kuna marriage zingine, mtu anakwenda kuoa tu, hata baba hakutuma ujumbe au familia hawakuenda kwa ujumbe au wapi. Mambo kama haya, hiyo si marriage, tunataka marriage ile tumekuenda ka ...(Inaudible) tumekwenda kuomba basi huyo ndio tumeleta aolewe ndiye tunajua, mali iende na mambo kama haya.

Com. Pastor Ayonga: Na wale ambao wamekuja bila nyinyi kufanya hivyo, tufanyeje?

Elijah arap Terer: Hiyo hatuwezi kutambua na hawezi kupata mali hapa. Ili marriage ambayo ilifanywa bila jamaa au family

kujua hiyo si marriage. Basi, asante sana.

Com. Pastor Ayonga: Asante mzee. Hebu kuja hapa mzee, ngoja uulizwe swali.

Com. Phoebe Asiyo: Nitakurudisha hapo kidogo nikuulize. Unasema mzee kwamba marriage hatuwezi kutambua kama watu hawakufika hapa nyumbani kufanya hiyo mipango. Sasa watoto wanasoma ngambo, wakikutana huko na wanataka kuona wakimaliza mashule yao na hawawezi kurudi hapa nyumbani kutengeneza mambo haya. Wakirudi siku ile wakimaliza masomo wanakuja kufanya kazi, tutawatambua au tutawakataa?

Elijah arap Terer: Wanaweza kuoana huko lakini lazima waje nyumbani kusema ya kwamba tumeoana na huyu hata kama ni Mzungu, sisi Wanandi tunasema bibi hana ukabila. Kama ni Mzungu ni bibi tu.

Com. Phoebe Asiyo: Bila kurudi nyumbani?

Elijah arap Terer: Lakini sasa kama wamefanya huko lazima waje nyumbani, tuketi chini na family, sisi tuna-confirm ya kwamba kweli alifanya hivyo kwa sababu hatukuweza kuenda huko kufanya uchumba huko. Kwa hivyo tutakubali walete tu tuzungumze tuseme tumefanya hii na tuseme sawa sawa halafu tunaweka sahihi.

Com. Phoebe Asiyo: Kwa maana sasa ukisema tumalize hata mimi nyumbani kwangu nitaumia maana vijana wangu wanaoa hapa na wako ng'ambo. Kwa hivyo wacha tu watu waoane lakini wakirudi nyumbani wamalize mipango hiyo...(Inaudible).

Com. Pastor Ayonga: Mzee, tusije tukajiuwa wakati watoto watu wako ng'ambo, watoto wetu huko wakipatana kitu kizuri umesema wakija hapa tutaanza kuwauliza sasa huyu baba yako yuko pande gani ilituanze kurekebisha. Tutarekebisha kama Katiba, ndiyo tutarekebisha. Huwezi kuwacha mtoto wako ambaye amekuletea wajukuu wanaokusalimia viziru umebeba halafu ukatae.

Elijah arap Terer: Hapana.

Com. Pastor Ayonga: Karibu weka sahihi.

Elijah arap Terer: Jambo lingine, iko moja nimekumbuka. Hii mambo ya kuoana na kuoana, bibi ameolewa tumekaa miaka mitano tumezaa mtoto mmoja halafu tumekosana aende. Akienda miaka kumi na azae na Mjalu, Mkikuyu, Mhindi, Mzungu analeta mchanganyiko halafu arudi nyumbani

Com. Pastor Ayonga: Na Mnandi mwingine?.

Elijah arap Terer: Hata Mnandi, halafu arudi nyumbani kusema niliolewa na Arap Terer kwa hivyo mimi naleta watoto wale ambao nimezaa huk. Hao watoto ni wa mama, anajua alizaa na nani, agawe watoto hawa kwa wale watu, wale nilizaa naye yule mmoja aliwacha hapa au kama walikuwa wawili basi, hawa ndio watoto wangu, Lakini wale wengine Wanandi wale wa zamani wanasema, kubali tu mzee ulioa, hawa ni watoto wako. Hakuna siku hizi, hiyo iishe.

Com. Phoebe Asiyo: Ngojea hapo kidogo. Sisi kwa Wajaluo, na hii mambo ni muhimi sana kwa Katiba, msichana akiolewa na tena aende nje wale watoto wote anazaa tunasema ni watoto wa ngombe, mpaka arudi nao kwa huyu mzee kwa maana pengine huyu mzee alikuwa hana bahati ya wanaume anapata wasichana tu. Sasa hawa watoto wa ngombe wanakuja kusaidia hapa, sasa ukisema tufunge hii pengine itaumiza miji ingine ambapo hawana mtoto wa kiume halafu inakuwa shida. Hebu tuwache haya mambo, kwa Katiba tusifunge mtu.

Elijah arap Terer: Hapana, mimi nataka nyinyi msikie ya kwamba hawa Wanandi wa siku hizi si Wanandi wa zamani na hawana mashamba kwa hivyo sikia sasa maoni, hiyo nimesema kwamba wale watoto wanaozaliwa huko wakae huko. Uliza hawa, wanasema nini? Si unasikia.

Com. Pastor Ayonga: Sasa hayo yalikuwa maoni ya mzee Terer, sasa Wanandi wengine pia wana mawazo yao. Lete mama kwanza tafadhali. Mzee ufanye dakika moja, sitaki kuona akina mama hapa kama wamechelewa. Asante mzee kwa kukubali wacha mama achukue kwanza. Endelea.

Patroba Kosgei: *Kainenyun ko Patroba Kosgei*

Translator: She is called Patroba Kosgei.

Patroba Kosgei: *Atindoi ngalek aeng che amwae.*

Translator: She has one or two words to say.

Patroba Kosgei: *Okot ndo ngololen kwonyik katiba ko kwonyik kora.*

Translator: We women even if they have talked about Katiba we are still women.

Patroba Kosgei: En ngalalet koboru kole kilen kiyechen.

Translator: The talk here seems to be inciting us so that we feel big.

Patroba Kosgei: Kisome kityok kegasech

Translator: We are asking that we are educated (Inaudible)

Patroba Kosgei: *Betusiechu kegonyiti kwonyi k che magitun kosir che kigitun.*

Translator: Single women nowadays are abit respected more than the married women.

Patroba Kosgei: *Okot kou yo overtakenigen karisiek konyolu konai kwonyik che mengechen kole neo boiyot.*

Translator: Like when the vehicles are traveling on the road and they overtake each other there is a way one must overtake, so what has been said here the young girls should know that the husband is still the head of the family.

Patroba Kosgei: *Ongetegiske asi kebe ta.*

Translator: Let us respect each other and then we shall succeed.

Patroba Kosgei: *kongoi*

Translator: Asante.

Com. Phoebe Asiyo: Asante sana mama tumeshukuru. Mzee unaweza kuendelea. Utasema jina lako halafu endelee.

John Maze: Mimi naitwa John Maze na yangu nitakayosema ni machache sana. Ninataka kusema kuhusu mambo ya ukulima wa mahindi. Tunaona shida inazidi sana kwa wakulima kwa maana tunanunua mbegu kwa bei ghali na tunalima kwa gharama kubwa.

Com. Phoebe Asiyo: Unataka tufanye nini kwa mkulima?

John Maze: Ndio mimi nasema sasa. Sasa kile kitu mimi naoni ni vizuri serikali kututafutia soko ya kuuza vitu vyote vya shamba kuliko sisi wenyewe tuseme tujitafutie. Sasa tunauza gorogoro ya mahindi shilingi kumi, tunakosa soko na wengine pia hawajui pahali watakwenda kuuza. Lakini tunasikia watu wengine wanakufa na njaa na hawa watu hawana hata ngombe wanipatie kubadilisha nayo. Sisi tunaona badala ya kupanda mahindi tunakosa hata fertilizer, ajambo serikali kama imechukua mahindi yetu kuuza tupate...

Com. Pastor Ayonga: Utuambie kitu cha kufanya, maoni?

John Maze: Tunataka serikali wanunue mahindi halafu iuze.

Com. Pastor Ayonga: Halafu point ingine?.

John Maze: Point ya pili nilikuwa nataka kusema maneno ya radio, tumeona radio imetuhaibisha sana hasa hii television.

Com. Pastor Ayonga: Okay, endelea.

John Maze: Siku moja tuliona kwa nyumba ya mwingine kama tunakula katika meza sasa akina mama walikuwa wanamenyana na kupigana uchi bila nguo, hata sisi tunawacha chakula na kutoroka. Nasema na hawa watu walilete hapa Kenya hii maneno ya nini? Na sisi tangu zamani tunaheshimiana.

Com. Pastor Ayonga: Kwa hivyo mzee unatakaje?

John Maze: Tunataka watu wa television waweke vitu vizuri vya maendeleo na ile ingine ya Wazungu watoe kabisa, hiyo imelete aibu kubwa kwa Kenya mzima.

Com. Pastor Ayonga: Asante, hiyo point mzee umeshaiweka na si point yako tu, watu wengi wameshaona hivyo. Kitu ambacho nataka ni kwamba tuwe na censorship, ni vitu gani watu huonyeshwa na ni vitu gani ambavyo havionyeshwi watu na vitu vya nyumba za cinema na vitu vya nyumba za watu. Kwa maana unakuwa unakula na watoto wako tena hata ulikuwa unaangalia hapa sasa tena unashindwa utoke uende, uzime au ufanye nini. Hiyo yote ni aibu. Asante sana mzee.

John Maze: Ya mwisho, nataka kuombo hii permit ya television ikatwe safari moja wakati inanunuliwa kwa sababu ni mbaya. Permit ikiisha kesho nasombwa kwa polisi. Ni vizuri kulipa safari moja sawa sawa na radio. Yangu imekwisha.

Com. Pastor Ayonga: Watu ambao walikuja hapa mapama, inawezekana ulikuja hapa asubuhi umeona watu wengine wamekuja nyuma yako, wameongea, wamekwenda na wewe bado hujaitwa na pengine jina lako liliitwa ulipotoka kidogo, unajua mtu hutoka kidogo kwa mambo mengine. Kuna mtu wa namna hiyo kati ya nyinyi mlioketi? Ambaye alikuja asubuhi na hajapata nafasi ya kuongea? Njoo pande huu, njoo hapa na ona saa, unajua tulikuja jua likiwa kule na sasa jua limerudi migongo yetu hapa na ni lazima tufanye haki. Hiyo si kusema kwamba wale ambao mmekuja saa hii mtoke nataka tu kujaribu kufanya haki. Nikiwapa dakika moja moja mtaweza? Lakini mnajua Wanandi, sisi Wanandi, tuna heshimu sana wazee. Mtu akiitwa boiyo, ni boiyo na anabaki kuwa hivyo na kama amesimama anaongea wanamwambia kwamba mzee kwa maana ni wewe nimewacha tu. Sasa nyingi naona ni ma-DOT.COM, mnisamehe kidogo. Mngojee tu kidogo hawa ni baba zenu, wengine ni babu. Kwa hivyo si tungefanya namna hivyo? Tukifuata mila za Wanandi lakini huyu mama nitamchanganya wakati wazee wawili wakiongea hapa, huyu mama lazima aingie ili aende nyumbani. Mzee dakika moja tu.

Thomas Rono: Asante sana. Kwa majina naitwa Thomas Rono. Yangu nataka kutaja kuhusu mambo ya cost sharing katika health centres au hospitali. Kwa mfano hapa Kabiyet Health Centre tunasanya pesa kutoka kwa wagonjwa halafu tunatuma zote ziende kwa district halafu baadaye tunafanya proposals kuomba hizo pesa zirudi ili tusaidie nayo wagonjwa lakini inakuwa na shida kupata hizo pesa. Kwa hivo maoni yangu ni kwamba, ningependa ikiwezekana hizo pesa tukishasanya tu-retain ile 75% halafu 25% iende kwa sababu.....(Inaudible).

Com. Pastor Ayonga: Point is made.

Thomas Rono: Thank you, nalikuwa na hiyo tu.

Com. Pastor Ayonga: Asante, mpe mzee mwingine yule ako nyuma yako. Kuja hapa na wewe mzee tunataka useme tu neno moja kama huyo.

William Sang: Ndiyo. Majina yangu ni William Sang. Mimi nataka kuzungumza juu ya Local Government. Mayor achaguliwe na watu na awe amehitimu form four.

Member of Parliament awe na cheti cha university ndio achaguliwe na kitu ingine tena nataka kuhusu Members of Parliament, siku hizi tunasikia kwamba hakuna quorum kwa Parliament na hawa watu wanaenda wapi?

Com. Phoebe Asiyo: Utuambie tu unataka namna gani?

William Sang: Kitu mimi nataka, kama hakuna quorum yale majina ya Wabunge ambao hawako katika Parliament waandikwe katika gazeti ili watu wasome kumbe fulani haendi Parliament.

Ya pili, nimeona kwamba Wabunge wakikaa sana kwa Bunge hawafanyi kazi vizuri. Kwa hivyo nasema Mjumbe awe kwa Parliament kwa two terms za miaka kumi.

Juu ya kotini, wakati wa wabeberu tulikuwa na tribunal ya court ambayo ilikuwa hapa Kabiyet.

Com. Phoebe Asiyo: Unataka turudishe hizo?

William Sang: Ndiyo, nataka turudishe hizo na ilikuwa inafanya kazi ya mashamba.

Com. Pastor Ayonga: Ndiyo tunajua, ikirudishwa itafanya hizo kazi ilizokuwa inafanya.

William Sang: Ndiyo irudishwe.

Com. Pastor Ayonga: Okay, ya mwisho?

William Sang: Ya mwisho, tunataka free treatment kwa sababu siku hizi watu hawawezi kununua dawa. Hayo ndiyo yangu.

Com. Pastor Ayonga: Asante sana.

Com. Phoebe Asiyo: Utakuja uweke sahihi.

Com. Pastor Ayonga: Nenda hapo ujiandikishe. Mama sema jina lako?

Martha Rono: Jina langu ni Martha Rono.

Com. Pastor Ayonga: Endelea.

Marth Rono: *Angololen nandi.*

Translator: I want to talk in Nandi so that they can hear or understand properly.

Marth Rono: *Atindoi ngolkyot agenge kityom*

Translator: She has one word to say.

Marth Rono: *Angalalen bik che kisir serkali.*

Translator: I am talking about the people who have been employed by the government.

Marth Rono: *bichon kigoemploen serkali.*

Translator: Those who have been employed by the government or whoever the employer is, knows the age of the employees.

Marth Rono: *Agobo chelewanetat bension yon kagoretiyan ago bwone kogakochelewonso kabisa.*

Translator: About the delay of the pensions, when one retires and the pension benefits come very late, sometimes they come after the person is dead.

Marth Rono: *Amache kechokyi asi komatar kenyt keonate nyolu okot koik arawet agenge.*

Translator: I am asking that they should speed up so that after one year or less or even a month.

Com. Phoebe Asiyo: Mama wewe useme hivi, yule mtu akitoka apewe wakati huo huo.

Martha Rono: Apewe na akuje nyumbani watoto wafurahie si ati akuje ndio pension baadaye.

Com. Pastor Ayonga: Kabisa, hapana ngoja mpaka watu wamekufa halafu, mtu anakufa ndipo pension inakuja.

Com. Phoebe Asiyo: You know, we are recommending ... (Inaudible).

Speaker: Mimi nilikuwa hapa kweli na mimi naomba tu.....(Inaudible).

Com. Pastor Ayonga: Hapana, ngoja kidogo, angalia, tafadhali nakuomba kwa heshima. Kama una jambo lolote ulisahau nenda uandike tutapewa kesho.

Speaker: Sijui kusoma.

Com. Pastor Ayonga: Watakusaidia, tafadhali.

